



## WIZARA YA AFYA



## BARAZA LA FAMASI

### **VIGEZO VYA KUZINGATIA KABLA KUFANYA MAOMBI YA KUFUNGUA FAMASI**

*(Made under Regulation 4&5 of the Pharmacy (Premises Registration) Regulations GN 269, 2020)*

#### **1.0 REJAREJA/COMMUNITY PHARMACY**

- (i) Hakikisha kuwa ukubwa wa jengo si chini ya mita za eneo 30 ( $30m^2$ ).
- (ii) Hakikisha kuwa umbali kutoka famasi ya karibu ya rejareja si chini ya mita 150 (150m)
- (iii) Hakikisha kuwa eneo unalotaka kufungua lipo umbali wa mita 100 kutoka sehemu zisizofaa kwa huduma za famasi, mfano: - bar, kituo cha mafuta, mifereji ya maji taka iliyowazi, madampo, gereji na umbali wa mita 50 kutoka maabara.
- (iv) Hakikisha kuwa umbali kutoka vituo vya kutolea huduma za afya vya Serikali unakuwa kama ifuatavyo;-
  - ✓ 500m kutoka Hospitali ya Taifa au Hospitali ya Kanda
  - ✓ 400m kutoka Hospitali ya Mkoa
  - ✓ 300m kutoka Hospitali ya Wilaya
  - ✓ 200m kutoka Kituo cha afya au Zahanati
- (v) Ukijiridhisha jaza fomu ya maombi ya ukaguzi wa awali kwa umakini **approval of location form – PCF.5a.**
- (vi) Lipia **TZS 100,000** kwa njia ya *Control number* kwa ajili ya ukaguzi na upewe risiti ya Baraza.

#### **2.0 JUMLA/WHOLESALE PHARMACY**

- (i) Hakikisha kuwa ukubwa wa jengo si chini ya mita za mraba 60 ( $60m^2$ ).
- (ii) Fuata hatua (iii) – (vii) kama ilivyo hapo juu.

#### **3.0 ZINGATIA YAFUATAYO:-**

- (i) Hutakiwi kufanya matengenezo yejote kabla haujafanyiwa ukaguzi wa awali.
- (ii) Baraza lina mamlaka ya mwisho kuamua eneo linalofaa kwa biashara ya famasi, na ni jukumu la mwombaji kuhakikisha kuwa anazingatia vigezo vilivyoweka na Baraza.
- (iii) Hakikisha namba za simu unazojaza zinapatikana muda wote.